**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# SERA YA TAIFA YA MAENDELEO NA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU


**IDARA YA USTAWI WA JAMII**

**WIZARA YA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**

**S.L.P. 1949**

**DAR ES SALAAM**

**JULAI, 2004**

## YALIYOMO

# MAANA YA MANENO

### SURA YA KWANZA:


1.0 Utangulizi ………………………………………………….. 1

1.1 Matukio Muhimu kabla ya Sera ………………………… 2

1.2 Hali ya Watu wenye Ulemavu Nchini…………………….. 3

1.2.1 Afya …………………………………………………… 4

1.2.2 Utambuzi wa Mapema wa Watoto wenye Ulemavu …… 4

1.2.3 Huduma ya Afya ya Akili ………………………………. 5

1.2.4 Watu Wenye Ulemavu na Ukimwi……………………….. 5

1.2.5 Elimu ………………………………………………….... 6

1.2.6 Mafunzo ya Stadi za Kazi ……………………………….. 6

1.2.7 Ajira …………………………………………………….. 7

1.2.8 Matunzo ………………………………………………… 7

1.2.9 Ajali na Fidia ……………………………………………. 8

1.2.10 Wazee wenye Ulemavu ………………………………….. 8

1.2.11 Nyenzo za Kujimudu ……………………………………. 8

1.2.12 Vikwazo katika Mazingira………………………………. 9

1.2.13 Uelimishaji wa Jamii ……………………………………. 9

1.2.14 Haki na Ulinzi wa Kisheria ……………………………… 9

1.2.15 Vyama vya Watu Wenye Ulemavu na vya Kuhudumia Watu wenye ulemavu……………………………………. 10

1.2.16 Ruzuku kwa vyama vya Watu wenye ulemavu na vinavyohudumia watu wenye ulemavu……………………. 11

1.2.17Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu…………….. 11


### SURA YA PILI:


2.0 Dira na Mwelekeo wa Sera………………………………… 12

2.1 Madhumuni ya Sera………………………………………… 12

2.2 Makundi Maalum ………………………………………… 13

**SURA YA TATU:**

**3.0 MATAMKO YA SERA**


3.1 Uelimishaji wa Jamii ………………………………………….. 14

3.2 Upatikanaji na Upashanaji wa Habari……………………….. 14

3.3 Huduma ya Afya ……………………………………………… 15

3.4 Utambuzi wa Mapema wa Watoto wenye Ulemavu………… 15

3.5 Huduma ya Afya ya Akili……………………………………… 16

3.6 Watu wenye Ulemavu na Ukimwi ………………………….. 16

3.7 Nyenzo za Kujimudu………………………………………….. 16

3.8. Elimu…………………………………………………………….. 17

3.9. Mafunzo ya Stadi za Kazi …………………………………….. 17

3.10 Ajira …………………………………………………………… 18

3.11 Uondoaji wa Vikwazo vya Ujenzi (accessibility)……………. 18

3.12 Matunzo……………………………………………………… 19

3.13 Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu katika Jamii (Community Based Rehabilitation – CBR)………………….. 19

3.14 Mchangamano Katika Jamii ………………………………. 20

3.15 Michezo ……………………………………………………… 20

3.16 Dini …………………………………………………………… 21

3.17 Usafiri na Usalama Barabarani……………………………. 21

3.18 Ajali na Fidia ……………………………………………… 21

3.19 Haki na Ulinzi wa Kisheria …………..…………………… 22

3.20 Mafunzo ya Watumishi …………………………………….. 22

3.21 Habari, Takwimu na Tafiti…………………………………. 23

3.22 Vyama vya Watu wenye Ulemavu…………………………. 23

3.23 Vyama vya Hiari vya Kuhudumia Watu wenye Ulemavu….. 23

3.24 Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye Ulemavu …………… 24

3.25 Ruzuku kwa Vyama vya Watu wenye Ulemavu na Vinavyohudumia watu wenye ulemavu……………………… 24

3.26 Ushirikiano wa Kimataifa……………………………………. 25

**SURA YA NNE:**

**4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU**

4.1 Serikali Kuu ………………………………………………….. 26

4.2 Serikali za Mitaa …………………………………………….. 26

4.3 Familia/Vijiji…………………………………………………. 27

4.4 Wakala za Hiari……………………………………………. 27

## DIBAJI

Tangu nchi yetu ipate Uhuru waka 1961 Serikali kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii imekuwa inatoa huduma kwa watu wenye ulemavu bila kuwa na sera timilifu. Kuwapo kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ni matokeo ya miaka mingi ya majadiliano baina ya Serikali na wadau. Pamoja na kutokuwapo kwa sera, Tanzania imekuwa inajihusisha na mipango mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa inayohusu masuala ya ulemavu. Kimataifa Tanzania imesaini mikataba mbalimbali kuhusu watu wenye ulemavu hususan mikataba ya Haki kwa watu wenye Ulemavu (1975), Haki za Mtoto (1989) na Haki na Fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu (1993).

Barani Afrika, Tanzania ni miongoni mwa inchi waasisi wa Mpango wa utekelezaji wa muongo wa Watu wenye Ulemavu na mwanachama wa Taasisi ya Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu (African Rehabilitation Institute – ARI). Pia tunashirikiana na mataifa mengine duniani kuhakikisha ukamilishaji wa Mkataba kuhusu Ulinzi na uboreshaji wa Haki na Heshima kwa watu wenye Ulemavu.

Hapa nchini serikali imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kampeni za chanjo ya kuzuia ulemavu utotoni (kwa mfano polio), kutunga sheria zinazolinda maslahi na kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu, kuwapo kwa swali kuhusu ulemavu katika sensa ya Taifa ya watu na makazi (2002) na mandalizi ya kuridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki na Fursa Sawa kwa Watu wenye Ulemavu.

Rasimu ya sera hii ilijadiliwa kwa kina na idadi kubwa ya wadau. Moja ya matukio ya kukumbukwa katika maandalizi ya sera hii ni hatua ya Vyama vya Watu wenye Ulemavu kutaka rasimu iliyowasilishwa Serikalini irejeshwe ili ifanyiwe marekebisho. Kwa hakika ilirejeshwa na matokeo ya hatua hiyo ni ubora wa sera hii tunayojivunia.

Sera inatoa mwongozo na inaweka vigezo vya utoaji huduma. Sera imejengwa kwa kuzingatia utamaduni wetu na inalenga katika kuleta maendeleo, haki na heshima kwa Watanzania wenye ulemavu.

Changamoto tuliyo nayo ni kutafsiri kwa vitendo matumaini yaliyomo kwenye Sera hii. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wadau wote, hasa watu wenye ulemavu wenyewe na taasisi/mashirika ya kimataifa tushirikiane kuhakikisha kwamba matarajio ya sera hii yanafikiwa.

Mwisho napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa maofisa wa Wizara yangu, vyama vya watu wenye Ulemavu na wale wote ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia katika kuwapo kwa sera hii.

Prof. Juma A. Kapuya (MB)
**WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO**

**Maana ya Maneno**

**(a) Ulemavu**

Ulemavu ni hali inayotokana na dosari mwilini au/na akilini ambayo inasababisha mtu kushindwa kutenda mambo ambayo kwa kawaida angetegemewa kuyaweza na hivyo kumletea mtu huyo kizuizi katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii. Kizuizi katika utendaji kinatokana pia na mfumo wa mtizamo wa jamii dhidi ya mtu huyo.

Ulemavu ni neno linalotumika kwa mapana kuainisha maeneo matatu muhimu yafuatayo:

- Hali ya tatizo kadri linavyoonekana (impairment)
- Upungufu wa uwezo wa kutenda/kufanya jambo kwa njia ya kawaida kulingana na hali yake (Disability).
- Kizuizi katika kutenda jambo (handicap) kutokana na hali ya ulemavu (Disability).

**(b) Mtu mwenye ulemavu (person with disability/disabled person):**

Ni mtu ambaye mategemeo yake ya kupata, kumudu na kujiendeleza katika kazi yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ulemavu unaotambulika mwilini, akilini, na/au mfumo wa mtizamo wa jamii dhidi ya mtu huyo.

**(c) Marekebisho (Rehabilitation):**

Huduma za marekebisho ni jumla ya juhudi za pamoja katika nyanja za afya, saikologia, elimu, kazi na jamii zenye madhumuni ya kuinua kiwango cha utendaji wa mtu mwenye ulemavu kwa kiasi kinachomwezesha kushiriki kwa ukamilifu katika maisha ya kila siku ya jamii yake.

Marekebisho ya watu wenye ulemavu yana sehemu zifuatazo:

- Marekebisho ya kimatibabu yenye shabaha ya kuongeza kiwango cha afya na utendaji kadri inavyowezekana.

- Marekebisho ya kisaikologia na kielimu yenye shabaha ya kumpa na kumwongezea elimu mtu mwenye ulemavu na pia kurekebisha msimamo wake wa akili kama ni lazima.
- Marekebisho ya kazi yenye shabaha ya kumtayarisha mtu mwenye ulemavu kwa ajili ya kufanya kazi.
- Marekebisho ya kijamii yenye shabaha ya kumwezesha mtu mwenye ulemavu kuishi na kufanya kazi kwa mchangamano katika jamii.

**(d) Utengemao (Resettlement).**

Hali ya utulivu wa maisha ya mtu mwenye ulemavu katika jamii kutokana na kutimizwa kwa mahitaji yake muhimu.

**(e) Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu katika jamii (Community Based Rehabilitation – CBR).**

Utaratibu unaoshirikisha jamii katika utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Jamii katika sera hii ina maana ya familia, Serikali ya Kijiji au Mtaa au kikundi chenye malengo na mahitaji yanayolingana.

**(f) Mchangamano (Intergration)**

Kiwango cha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maisha na kazi za jamii sawa na wasio na ulemavu.

**(g) Haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu (equalization of opportunities for persons with disabilities).**

Upatikanaji wa haki, huduma na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu sawa na wasio na ulemavu.

**(h) Kazi (work)**

Kazi katika sera hii inamaanisha shughuli yoyote halali itakayomwezesha mtu mwenye ulemavu kujitegemea.

**(i) Misaada/nyenzo za kujimudu (Technical Aids/Appliances)**

Vifaa vinavyomwongezea uwezo mtu mwenye ulemavu kwa kuimarisha viungo vilivyopungukiwa nguvu (orthotics) au kwa kufidia viungo visivyokuwepo (prosthetics). Katika sera hii "nyenzo za kujimudu" ni pamoja na vifaa au nyenzo zinazomwongezea mtu mwenye ulemavu uwezo wa kumudu mazingira.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi.

Ulemavu ni hali inayotokana na dosari ya kimwili au ya kiakili ya muda mfupi au ya kudumu ambayo inampunguzia mtu uwezo na fursa sawa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika jamii. Upungufu huo unaweza kuchochewa na mazingira na mtizamo wa jamii kuhusu ulemavu.

Katika jamii yetu na kwingineko duniani hali ya mtu kuwa na ulemavu inaambatana na unyanyapaa unaotokana na mila zilizopitwa na wakati. Kutokana na hali hii watu wenye ulemavu wanaonekana kuwa ni tegemezi wasio na uwezo na wanaostahili kusaidiwa na watu wasio na ulemavu katika kumudu maisha yao. Mtizamo huu unasababisha kutengwa kwa watu wenye ulemavu katika maisha ya kila siku ya jamii inayowazunguka. Mtizamo huu ni hasi na unakwenda kinyume na haki za kimsingi za binadamu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza kwamba binadamu wote ni sawa na kwamba wanastahili kupata haki sawa bila kujali rangi, kabila, jinsi na dini.

Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 20 Disemba 1948 ulipitisha Azimio Na. 27 (a) (III) ambalo linaeleza kwamba binadamu wote wamezaliwa huru wakiwa sawa katika haki na kustahili heshima. Kwa kadri ya Azimio hili binadamu ana haki ambazo anastahili kuzipata toka kwa jamii na pia ana wajibu kwa jamii. Haki hizo ni za kuitumia jamii, na rasilimali zake kwa ajili ya maendeleo na usalama wake. Kwa kuwa mtu mwenye ulemavu ni binadamu naye ana haki hizo pia.

Licha ya Azimio hili Umoja wa Mataifa umepitisha maazimio kadhaa kuhusu haki na usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

## 1.1. Matukio muhimu kabla ya Sera.

Awali, utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu haukuwa na sera maalum bali ulikuwa ukifanywa kwa kadri matatizo yalivyojitokeza na maelekezo mbalilmbali ya Serikali na chama tawala (kwa mfano Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na Azimio la Arusha). Kutangazwa kwa mwaka wa 1981 kuwa ni mwaka wa Kimataifa wa Watu Wenye Ulemavu, kulileta vuguvugu lililoifanya Serikali kutayarisha miongozo na kupanga mikakati ya utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Miongozo na mikakati hiyo ni pamoja na:-

**(a) Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 19 wa 1981:**

Waraka huu una sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza unaelezea matatizo yaliyodhihirika katika utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu kwa sababu ya kutokuwepo miongozo. Sehemu ya pili imegawa majukumu ya matunzo kwa watu wenye ulemavu kwa mamlaka na taasisi mbalimbali, familia,ndugu, vijiji, Serikali na Wakala za Hiari. Waraka huu unasisitiza shabaha ya utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu ambayo ni kulinda usalama na utu wao.

**(b) Sheria Na. 2 ya 1982: Ajira ya watu wenye ulemavu.**

Sheria hii ilitokana na Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 19 wa 1981. Madhumuni makuu ya sheria hii ni:

- Kuimarisha huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kutenga nafasi za ajira kwa ajili yao.
- Kuanzisha Baraza la Taifa la Ushauri wa huduma kwa watu wenye ulemavu lenye jukumu la kumshauri Waziri anayehusika na huduma kwa watu wenye ulemavu kuhusu huduma hizo.

**(c) Sheria Na. 3 ya 1982: Matunzo ya watu wenye Ulemavu na Wasiojiweza.**

Sheria hii inatokana pia na Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 19 wa 1981. Madhumuni makuu ya sheria hii ni kuimarisha huduma ya matunzo kwa watu wenye ulemavu na wasiojiweza kwa kuweka wazi mamlaka zenye jukumu la kutoa matunzo (familia, ndugu, vijiji, Serikali na Wakala za Hiari).

**(d) Serikali kuvitambua vyama vya Watu Wenye Ulemavu:**

Mwaka 1981 Serikali ilichukua hatua muhimu ya kuvitambua rasmi vyama vya Watu Wenye Ulemavu. Serikali inatambua kwamba Vyama vya watu wenye ulemavu ni vielelezo vya umoja wao, nguvu ya pamoja ya kutetea maslahi yao na ni vyombo vya uwakilishi.

## 1.2 Hali ya Watu wenye Ulemavu Nchini.

Sensa ya Taifa ya watu na makazi ya mwezi Agosti – Septemba imejumuisha vipengele mahususi kwa ajili ya kupata taarifa zinazowahusu watu wenye ulemavu. Taarifa rasmi kwa sasa hazijapatikana.

Hata hivyo kutokana na hesabu za uwiano kama zilivyoanishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mtu mmoja miongoni mwa watu kumi katika jamii ni mwenye ulemavu. Hivyo Tanzania inayokadiriwa kuwa na takriban watu 34,569,232 (2002) ina watu wenye ulemavu wapatao 3,456,900 waliogawanyika ifuatavyo:-

| | **Asilimia ya wenye Ulemavu** | **Idadi ya wenye Ulemavu** |
|---|---|---|
| Wenye ulemavu wa viungo | 28% | 967,932 |
| Wasioona | 27% | 933,363 |
| Viziwi | 20% | 691,380 |
| Wenye ulemavu wa akili | 8% | 276,552 |

| | | |
|---|---|---|
| Wenye ulemavu mchanganyiko | 4% | 138,276 |
| Wenye ulemavu wengine | 13% | 449,397 |
| **Jumla** | **100%** | **3,456,900** |

Kuporomoka kwa uchumi kunakotokana na utandawazi, madeni na mabadiliko katika mfumo wa uchumi duniani kumeathiri maisha ya watu kiuchumi na kijamii. Nchini Tanzania mabadilko ya kiuchumi yameathiri upatikanaji wa huduma mbalimbali kama vile za afya, elimu na upatikanaji wa ajira. Hali hii imeathiri zaidi maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu hasa katika maeneo yafuatayo:

### 1.2.1 Afya:

Pamoja na jitihada za kitaifa za kuweka kipaumbele katika kutoa huduma za chanjo kwa watoto, huduma za afya kwa ujumla hazikidhi mahitaji ya wananchi na hasa watu wenye ulemavu.

Asilimia kubwa ya wananchi wanaopata ulemavu hutokana na sababu za kiafya, umaskini, mazingira duni, lishe duni, ukosefu wa chanjo kwa watoto dhidi ya magonjwa yanayoleta ulemavu na matunzo duni kwa akina mama wajawazito ni miongoni mwa sababu za watu kupata ulemavu.

Magonjwa kwa akina mama wajawazito au matatizo wakati wa kujifungua husababisha ulemavu kwa mama mwenyewe au mtoto atakayezaliwa. Upatikanaji wa huduma za ushauri na matibabu kwa akina mama wajawazito hupunguza kasi ya ulemavu katika jamii. Umaskini walionao watu wenye ulemavu na familia zao unawafanya washindwe kupata nyenzo za kujimudu ambazo zingewawezesha kufikia vituo vya afya kwa urahisi. Kutokana na hali hiyo watu wenye ulemavu walio wengi hasa wa vijijini wanashindwa kupata huduma za afya wanazostahili.

### 1.2.2 Utambuzi wa Mapema wa Watoto wenye Ulemavu.

Upo umuhimu wa kufanya utambuzi wa mapema wa watoto wenye

ulemavu. Utambuzi wa mapema unatoa nafasi ya ama kuondoa hali ya ulemavu au kupunguza makali ya ulemavu ukubwani. Kwa bahati mbaya hapa nchini hakuna mpango wa kitaifa wa utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu unaowawezesha wananchi hasa vijijini kuwatambua watoto wenye ulemavu mapema.

Isitoshe kufichwa kwa watoto wenye ulemavu kutokana na mila na desturi za jamii husika zinawafanya wawe katika mazingira magumu zaidi ya kukosa huduma.

### 1.2.3 Huduma ya Afya ya Akili.

Kutokana na sababu mbalimbali za kijamii na kiuchumi baadhi ya wananchi wamekuwa wakipata matatizo ya afya ya akili. Watu hao wanaishi katika mazingira yanayohatarisha usalama wao na watu wengine na inaonekana kuwa hakuna mamlaka yenye jukumu la kuwatambua na kuwapatia msaada wa mapema.

### 1.2.4 Watu wenye Ulemavu na Ukimwi.

Watu wenye ulemavu wana matamanio ya kimapenzi kama watu wengine. Jitihada za kuhamasisha jamii dhidi ya Ukimwi haziwashirikishi watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu walio wengi ni maskini na hawana elimu ya kutosha hivyo kuwafanya washindwe kupata taarifa kuhusu Ukimwi.

Taratibu nyingi za uhamasishaji hazikidhi haja ya makundi maalum ya watu wenye ulemavu, kwa mfano wasioona hakuna maandishi ya nukta nundu na viziwi hakuna wakalimani wa lugha ya alama.

Hali ya kukosa nyenzo za kujimudu kunawafanya watu wenye ulemavu kukosa faida ya uhamasishaji dhidi ya ukimwi na hivyo kuwa katika hatari ya kuambukizwa.

### 1.2.5 Elimu.

Imedhihirika kwamba watoto wenye ulemavu wanakabiliwa na mtizamo hasi wa watu wanaowazunguka (negative attitude). Hivyo kuwa na msimamo wa kiakili unaowanya washindwe kukabiliana na mazingira yao kiukweli.

Elimu ni muhimu kwa maisha na maendeleo ya binadamu, hata hivyo elimu peke yake huwa ndio uwezo (faculty) anaotegemea mtu mwenyeulemavu katika kutawala mazingira kwa maendeleo yake baada ya uwezo mwingine kuzuiwa na ama kupunguzwa na ulemavu. Mtizamo hasi wa jamii dhidi ya watu wenye ulemavu huchangia watoto wenye ulemavu kutopata elimu ambapo baadhi ya wazazi na ndugu huwaona watoto hao kama mzigo na hivyo kuamua kutowapeleka shule. Mfumo wa elimu nchini pia hautoi fursa na nafasi sawa kwa watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Kutokana na hali zao watoto wenye ulemavu wanashindwa kumudu mazingira ya shule hivyo kushindwa kuandikishwa kujiunga na darasa la awali/kwanza. Shule takriban zote za awali/msingi/sekondari na vyuo vya elimu ya juu vimejengwa bila kuzingatia mahitaji maalumu ya watoto wenye ulemavu. Mafunzo ya waalimu na mitaala ya shule kadhalika haizingatii mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu, kwa mfano matumizi ya lugha ya alama na maandishi ya nukta nundu. Kutokana na mazingira haya idadi ya watoto wenye ulemavu wanaoandikishwa darasa la kwanza ni chini ya asilimia moja. Idadi ni ndogo zaidi katika shule za sekondari na vyuo.

### 1.2.6 Mafunzo ya Stadi za Kazi.

Maisha ya binadamu yanategemea utendaji wake wa kazi. Mafunzo ya stadi za kazi yanampa mtu mwenye ulemavu nafasi ya kupata ajira. Pamoja na umuhimu huo wa mafunzo mazingira ya vyuo vinavyotoa mafunzo ya stadi za kazi hayazingatii mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu hivyo kuwanyima fursa ya kujiunga. Mazingira hayo ni pamoja na majengo ambayo hayakidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu (ngazi, milango

myembamba, vyoo), mitaala na waalimu wasio na taaluma ya kufundisha watu wenye ulemavu. Isitoshe kipato duni kinawafanya watu wenye ulemavu washindwe kuchangia gharama za mafunzo. Mafunzo yanayotolewa na vyuo vya watu wenye ulemavu hayamuwezeshi muhitimu kuata ajira.

### 1.2.7 Ajira.

Kazi ni kielelezo cha utu. Kufanya kazi kunamwezesha binadamu kujitegemea hivyo kupata heshima katika jamii. Kutokana na utamaduni wetu kazi imekuwa ikilinganishwa na ukamilifu wa viungo vya mwili au akili. Kutokana na hali zao watu wenye ulemavu wanaonekana na jamii kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi. Kutokana na mtizamo huo wa jamii watu wenye ulemavu wenyewe wanajiona kama hawana uwezo wa kufanya kazi. Ujumla wa hali hii unafanya upatikanaji wa ajira kwa watu wenye ulemavu kuwa mgumu. Kwa kutambua ugumu huo Serikali ilitunga sheria namba 2 ya 1982 (Ajira kwa watu wenye ulemavu) ambayo hata hivyo haijaweza kukidhi mahitaji ya ajira kwa watu wenye ulemavu kutokana na mabadiliko ya uchumi duniani na utandawazi.

### 1.2.8 Matunzo.

Katika jamii yoyote ile kunakuwepo na kundi la watu ambao uwezo wao wa kujimudu kimaisha umepungua au haupo kabisa na hakuna mtu wa kuchukua jukumu hilo. Hali hii husababishwa na mazingira yafuatayo:-

(i) Ndugu kushindwa kutoa matunzo kutokana na hali yao kuwa duni au kutotaka kumtunza kwa sababu ya kutomthamini mtu mwenye ulemavu.

(ii) Mtu kutokuwa na mawasiliano na ndugu/jamaa zake kutokana na kuondoka sehemu aliyozaliwa kwa muda mrefu kwa mfano kwenda kutafuta ajira mbali na eneo lake la asili hivyo anapofikia umri wa kuhitaji matunzo anakosa mtu wa kumtunza.

(iii) Hali ya ulemavu mkubwa inayohitaji uangalizi wa muda wote inasababisha ndugu wa mtu mwenye ulemavu kushindwa kumhudumia na hivyo huduma ya matunzo katika makazi inakuwa muhimu kwa mtu huyo.

Huduma ya matunzo kwa watu wenye ulemavu nchini hairidhishi. Kuna upungufu mkubwa wa vifaa na nyenzo na wahudumu wengi hawana ujuzi wa kutosha. Hivyo huduma inatolewa katika kiwango cha chini. Utaratibu wa Serikali Kuu kuwa mwendeshaji wa makazi unaifanya huduma hii kuwa mbali na walengwa. Mwelekeo wa sasa wa Serikali kuu kutoa majukumu kwa Serikali za Mitaa na wakala za hiari unatoa nafasi ya kuboreka kwa huduma katika makazi.

**1.2.9 Ajali na Fidia:**

Maendeleo ya kiuchumi yanaambatana na kukua kwa viwanda na urahisi wa njia za usafiri. Ajali kwenye vyombo vya usafiri na sehemu za kazi zimekuwa ni chanzo kikubwa cha ulemavu.

Pamoja na kuongezeka kwa idadi ya watu wenye ulemavu kutokana na ajali upo ugumu wa kupata fidia kwa waathirika. Pale fidia inapotolewa huwa ni ndogo na isiyolingana na uzito wa tatizo la ulemavu.

**1.2.10 Wazee wenye Ulemavu.**

Uzee unaambatana na upungufu wa uwezo wa kimwili na kiakili. Uzee unaombatana na ulemavu unamweka mzee huyo katika hali ya kushindwa kushiriki katika kujiletea maendeleo yake na ya jamii hivyo kumweka katika mazingira magumu katika maisha.

**1.2.11 Nyenzo za Kujimudu.**

Watu wenye ulemavu wanahitaji nyenzo mbalimbali ili kuimarisha au kuwa badala ya kiungo/viungo vyenye ulemavu. Nyenzo za kujimudu ni pamoja na henzerani nyeupe (white canes), shimesikio (Hearing Aid), viatu

maalum, ubao wa kuandikia maandishi ya nukta nundu (braille writing frames), kofia na miwani. Nyenzo nyingine ni pamoja na baiskeli au pikipiki za magurudumu matatu, gari maalum, mashine ya kupigia chapa maandishi ya nukta nundu. Pamoja na umuhimu wa nyenzo hizo upatikanaji wake unakuwa ni mgumu.

### 1.2.12 Vikwazo katika Mazingira.

Hali ya kuwa na ulemavu ina uhusiano mkubwa na mazingira. Takriban majengo yote ya umma yamejengwa kwa kuzingatia mahitaji ya watu wasio na ulemavu. Huduma za ngazi, milango na vyoo hazitoi fursa kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali kuzitumia kwa urahisi. Kadhalika ujenzi wa barabara na muundo wa vyombo vya usafiri hautoi fursa ya matumizi ya watu wenye ulemavu. Hali hii inafanya mtu mwenye ulemavu ashindwe kuwasiliana na mazingira yake.

### 1.2.13 Uelimishaji wa Jamii.

Kumekuwepo na mtizamo hasi dhidi ya ulemavu na watu wenye ulemavu katika jamii. Kutokana na mila na desturi, kuzaliwa kwa mtoto mwenye ulemavu katika jamii kunahusishwa na imani za kiuchawi au balaa. Kutokana na hali hiyo jamii imekuwa na mtizamo hasi ambao ni miongoni mwa vizuizi vikubwa vinavyosababisha kutengwa kwa watu wenye ulemavu katika jamii na hivyo kuwafanya wasishiriki kwa ukamilifu katika shughuli za kujiletea maendeleo yao na ya jamii. Mara nyingi ulemavu unaonekana kuwa ni tatizo na mtu mwenye ulemavu anaonekana kuwa ni asiyejiweza na tegemezi.

### 1.2.14 Haki na Ulinzi wa Kisheria.

Sheria zilizopo zimetungwa bila kuzingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu. Kwa misingi hiyo utekelezaji wa sheria hizo haunufaishi watu wenye ulemavu kwa mfano sheria ya ujenzi isiyozingatia uwekaji wa mtelemko (ramp) badala ya ngazi ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kuingia/kutoka kwenye majengo kwa urahisi. Sheria ya habari isiyozingatia

upatikanaji taarifa kwa njia zinazoeleweka kwa watu wenye ulemavu (lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu).

Pamoja na sheria zisizozingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu yapo mapungufu makubwa katika Sheria zilizotungwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

**Sheria hizo ni:**

(i) Sheria ya Ajira kwa Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 1982 Sheria hii ilitungwa kwa minajili ya kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata ajira na kuelekeza asilimia 2% ya watumishi 50 mahali pa kazi wawe watu wenye ulemavu. Kutokana na mabadiliko ya kisiasa kiuchumi na utandawazi vipengele vya sheria vimepitwa na wakati.

(ii) Sheria Na. 3 ya 1982 matunzo kwa watu wenye ulemavu. Sheria hii inatoa majukumu kwa Halmashauri za wilaya kumiliki na kuendesha makazi ya watu wenye ulemavu. Pamoja na kupewa majukumu hayo haujaandaliwa utaratibu wa kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu hayo.

### 1.2.15 Vyama vya Watu wenye Ulemavu na vya Kuhudumia Watu wenye Ulemavu.

Utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu unahitaji rasilimali nyingi. Ushiriki wa taasisi zisizo za Serikali katika utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu unasaidia Serikai kutoa huduma timilifu kwa wananchi wake. Pamoja na umuhimu huo Wizara inayosimamia huduma hii inashindwa kuratibu na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Wakala zisizokuwa za Serikali (NGOs) kwa kuwa usajili wa taasisi hizo hauhusishi Wizara inayohusika na huduma hiyo.

### 1.2.16 Ruzuku kwa Vyama vya Watu wenye Ulemavu na vinavyohudumia watu wenye ulemavu.

Vyama vya watu wenye ulemavuni msngi wa mshikamano na sauti ya uwakilishi wao katika jamii. Uwezo wao wa kuviendesha vyama hivyo ni mdogo kutokana na umaskini walionao na msaada mdogo wanaoupata toka kwa jamii. Vyama vya kuhudumia watu wenye ulemavu havina uwezo wa kifedha na vinategemea misaada toka kwa wafadhili. Serikali ina wajibu wa kuvisaidia vyama hivi kwa hali na mali ili viweze kutekeleza wajibu wao katika jamii.

### 1.2.17 Mfuko wa Maendeleo kwa watu wenye Ulemavu.

Watu wenye ulemavu ni miongo ni mwa watu maskini katika Jamii. Maisha yao yanaambatana na vikwazo ikiwa ni pamoja na kutengwa. Ushiriki wao katika uzalishaji mali ni mdogo. Mikakati iliyopo ya kuondoa umaskini haijawashirikisha kikamilifu watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu hawajahamasishwa vya kutosha kuweza kufaidika na mifuko ya kuendeleza makundi maalum kama vile vijana na wanawake.

# SURA YA PILI

## 2.0 Dira na mwelekeo wa Sera.

Tanzania ni nchi inayojengwa kwa kufuata misingi ya usawa na haki kwa wananchi wote. Kila mwananchi ana haki sawa kisheria ya kushiriki kikamilifu katika mambo muhimu yanayomhusu yeye mwenyewe na jamii nzima kwa ujumla. Kila mwananchi ana haki ya kupata mahitaji ya msingi. Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata mahitaji ya msingi sambamba na wananchi wengine wasio na ulemavu. Pamoja na kasoro inayoambatana na ulemavu, watu wenye ulemavu ni rasilimali na nguvu kazi ambayo haijatambulika na kutumiwa ipasavyo kwa ajili ya maendeleo yao na ya jamii. Upo umuhimu wa kutambua uwezo na vipaji maalum vya watu wenye ulemavu na kuweka mikakati madhubuti ya kuviendeleza.

Sera ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu inalenga katika kujenga mazingira muafaka kwa watu wenye ulemavu kujiletea maendeleo na kutumia rasilimali zilizopo kuboresha huduma kwao.

## 2.1 Madhumuni ya Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu.

Kwa mwelekeo huu sera hii inajengwa kwa lengo la kuboresha maisha ya Watu Wenye Ulemavu katika jamii kwa kutekeleza yafuatayo:

- Kuchochea maendeleo ya watu wenye ulemavu.
- Kuwezesha familia za watu wenye ulemavu kumudu makali yatokanayo na matunzo ya mtu mwenye ulemavu.
- Kurekebisha sheria zisizolinda na kutoa haki kwa watu wenye ulemavu.
- Kutoa huduma bora kwa Watu Wenye Ulemavu.
- Kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa masuala muhimu katika jamii.

- Kuwezesha familia za watu wenye ulemavu na jamii kwa ujumla kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa masuala muhimu yanayowahusu watu wenye ulemavu.

## 2.2 Makundi Maalum.

Katika kutoa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu sera hii itatilia mkazo Kwenye makundi yafuatayo:

- Wanawake wenye ulemavu.
- Watoto wenye ulemavu.
- Wazee wenye ulemavu.

## SURA YA TATU

### 3.0 MATAMKO YA SERA.

### 3.1 Hoja ya Sera: Uelimishaji wa Jamii.

Msimamo hasi dhidi ya watu wenye ulemavu ni kizuizi katika maendeleo yao. Msimamo huo unasababisha kutengwa kwa watu wenye ulemavu katika jamii na hivyo kuwafanya washindwe kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo yao na ya jamii kwa ujumla. Upo umuhimu wa kurekebisha mtizamo huu kwa kuwapa nafasi watu wenye ulemavu ili waishi maisha ya kuzalisha na kujitegemea kama wananchi wengine.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu utakaoshirikisha wadau na watu wenye ulemavu wenye kuelimisha jamii ili itambue mahitaji, haki, uwezo na mchango wa watu wenye ulemavu katika jamii. |

### 3.2 Hoja ya Sera: Upatikanaji na Upashanaji wa Habari.

Upatikanaji wa habari na taarifa kuhusu huduma na maendeleo ya watu ni sehemu muhimu ya utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu.

Maendeleo ya watu wenye ulemavu na ushiriki wao katika maisha ya kila siku yanategemea kwa kiasi kikubwa habari na taarifa walizonazo. Kwa bahati mbaya utaratibu uliopo wa utoaji huduma hautoi nafasi kwa watu wenye ulemavu na ndugu zao kupata taarifa muhimu kuhusu huduma zilizopo na namna zinavyopatikana. Hali hii inawaweka watu wenye ulemavu katika mazingira ya kukosa huduma na fursa ya kujiletea maendeleo yao.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| (i) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba watu wenye ulemavu, familia na taasisi zinazohudumia watu wenye ulemavu zinapata taarifa muhimu kuhusu huduma zilizopo.<br>(ii) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba taarifa muhimu kwa umma zinatolewa katika lugha na maandishi yanayoeleweka kwa makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu (lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu). |

### 3.3. Hoja ya Sera: Huduma ya Afya.

Mara nyingi ulemavu unatokana na matatizo ya kiafya, umasikini, mazingira duni, mila na desturi za jamii husika. Pamoja na hali hii asilimia kubwa ya ulemavu unaweza kuzuiliwa kwa kuboresha mazingira na kuzingatia taratibu za kimsingi za afya. Hivyo utoaji wa huduma za afya ya msingi hauna budi kutilia mkazo huduma za kinga na uelimishaji jamii kuhusu uboreshaji wa mazingira, lishe na elimu ili kuwawezesha wananchi kujikinga dhidi ya magonjwa na desturi zinazosababisha ulemavu.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utaratibu mzuri uliopo sasa wa utoaji huduma ya afya ya msingi na uelimishaji jamii uimarishwe. |

### 3.4 Hoja ya Sera: Utambuzi wa Mapema wa Watoto wenye Ulemavu.

Utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu ni hatua muhimu ya kinga ya makali ya ulemavu ukubwani. Utambuzi wa mapema unaoenda sambamba na tiba una nafasi ya kuondoa kabisa ulemavu au kupunguza makali na madhara yake ukubwani. Kwa hiyo katika hali ya kawaida utambuzi wa mapema ni jawabu la kudumu la matatizo ya ulemavu ukubwani. Pamoja na umuhimu wa huduma hii kwa watoto wenye ulemavu ni asilimia ndogo sana inayofikiwa.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu unaoshirikisha wadau wa kufanya ufanya utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu. |

### 3.5 Hoja ya Sera: Huduma ya Afya ya Akili.

Kutokana na matatizo ya kiuchumi, kisaikolojia na maradhi baadhi ya wananchi wanapata matatizo ya kiakili. Mazingira wanayoishi watu wenye matatizo ya akili yanahatarisha usalama wao na watu wengine. Upatikanaji wa huduma ya afya hauna budi kuzingatia utambuzi na upatikanaji wa msaada wa mapema kwa wagonjwa wa akili.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu utakaoshirikisha taasisi za ulinzi na afya/huduma za jamii itaweka utaratibu utakaowawezesha watu wenye matatizo ya afya ya akili (mental health) kutambuliwa na kupata huduma ya afya mapema. |

### 3.6 Hoja ya Sera: Watu Wenye Ulemavu na Ukimwi.

Watu wenye ulemavu wana matamanio na hisia za kimapenzi kama watu wengine wasio na ulemavu. Jitihada za kuihamasisha/kuelimisha jamii juu ya janga la Ukimwi haziwafikii watu wengi wenye ulemavu mathalani mbinu za uelimishaji zinawacha nje baadhi ya wenye matatizo ya kuona na kusikia ambao uelewa wao unategemea kugusa na lugha ya alama. Upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba mbinu zinazotumika kuelimisha jamii kuhusu Ukimwi zinafikisha ujumbe kwa watu wenye ulemavu.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| (i) Utaweka utaratibu utakaohakikisha kwamba mbinu za uelimishaji kuhusu Ukimwi zinalenga katika kutoa ujumbe kulingana na mahitaji ya watu wenye ulemavu. |

### 3.7 Hoja ya Sera: Nyenzo za Kujimudu.

Ufanisi wa maisha ya kila siku ya mtu mwenye ulemavu unategemea sana upatikanaji wa nyenzo za kujimudu anazotumia katika kuwasiliana na mazingira. Pamoja na umuhimu wa nyenzo hizo upatikanaji wake ni mgumu na watu wenye ulemavu na ndugu zao hawapati taarifa za kutosha kuhusu wapi pakuzipata. Pale nyenzo hizo zinapopatikana zinakuwa ghali

na kufanya watu wengi wenye ulemavu kushindwa kuzinunua. Kutokana na kukosa nyenzo hizo watu wenye ulemavu wanashindwa kumudu mazingira hivyo kunyimwa fursa ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo yao na ya Taifa.

**Tamko la Sera:**

(i) Kwa kushirikiana na vyama vya watu wenye ulemavu utawekwa utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu upatikanaji wa nyenzo za kujimudu.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itagharamia upatikanaji wa nyenzo za kujimudu kwa wasio na uwezo.
(iii) Serikali itagharamia upatikanaji wa nyenzo hizo itakapodhirika kwamba mtu mwenye ulemavu hawezi kuzilipia na wala hana mhisani anayeweza kugharamia kwa niaba yake.
(iv) Serikali itatoa msamaha wa kulipia ushuru kwa nyenzo zote za kujimudu kwa watu wenye ulemavu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi. AidhaSerikali haitatoza kodi nyenzo zinazotengenezwa nchini.
(v) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba nyenzo bora na za bei nafuu zinazalishwa nchini.

## 3.8 Hoja ya Sera: Elimu.

Elimu ina umuhimu wa pekee kwa watoto wenye ulemavu. Elimu humpa nafasi mtoto mwenye ulemavu ya kujiendeleza na hivyo kumwezesha kutawala mazingira kwa maendeleo yake. Sera ya elimu nchini inasisitiza upatikanaji wa elimu ya awali na ya msingi kwa watoto wote wenye umri wa miaka saba (7) na kwamba watoto wenye ulemavu watapewa kipaumbele. Pamoja na azma hii mfumo wa elimu hautoi fursa kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu bila vipingamizi.

**Tamko la Sera:**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itaweka mazingira yatakayohakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanapata elimu jumuishi kwa kuzingatia mahitaji yao maalum.

## 3.9 Hoja ya Sera: Mafunzo ya Stadi za Kazi.

Mafunzo ya stadi za kazi ni muhimu katika kumwezesha mtu mwenye Ulemavu kujiendeleza. Mafunzo yanayotolewa katika vyuo vya ufundi kwa watu wenye ulemavu yana upungufu kwa kuwa hayalengi katika kumwandaa ili ajitegemee na kushiriki katika maendeleo yake na Taifa.

Pamoja na ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo visivyokuwa vya watu wenye ulemavu, mazingira ya utoaji huduma ya taasisi hizo hayajumuishi mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu.

**Tamko la Sera:**

(i) Itaandaliwa programu ya utambuzi na uendelezaji wa vipaji maalum vya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaboresha mazingira na mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu.

(iii) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba mafunzo ya stadi za kazi yanatolewa katika vyuo vya mafunzo uchangamano.

## 3.10 Hoja ya Sera: Ajira.

Kazi ni muhimu katika maendeleo ya binadamu. Licha ya kumwezesha mtu kujitegemea kazi pia inaleta heshima. Watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi ya watu walio maskini zaidi nchini. Hali hii inatokana na wengi wao kushindwa kupata ajira kutokana na hali zao na ushindani uliopo kwenye soko la ajira.

**Tamko la Sera:**

**(i) Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata nyenzo zitakazo wawezesha uanzisha na kuendeleza miradi ya uzalishaji mali.**

**(ii) Serikali kwa ushirikiana na wadau itafanya mapitio ya sheria ya ajira (Na. 2) ya mwaka 1982.**

## 3.11. Hoja ya Sera: Uondoaji wa Vikwazo vya Ujenzi (Accessibility).

Ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maisha na kazi za jamii unategemea kwa kiasi kikubwa uwezo wa mtu huyo wa kumudu mazingira. Matumizi ya nyenzo za kujimudu kama vile henzerani nyeupe, viti vya magurudumu na baiskeli za magurudumu matatu zinarahisisha uwezo wa mtu mwenye ulemavu kumudu mazingra. Kwa upande mwingine, ujenzi wa majengo ya umma, barabara, viwanja vya michezo na uwekaji wa vyombo vya huduma kama vile simu za umma, mabomba ya maji na uchimbaji mitaro hauzingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu hivyo kuwafanya washindwe kumudu na kuwasiliana na mazingira yao kwa urahisi.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu utakaoshirikisha wadau kuhakikisha kwamba ujenzi na uwekaji wa vyombo vya huduma unazingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. |

### 3.12 Hoja ya Sera: Matunzo.

Katika jamii yoyote ile kunakuwepo na kundi la watu ambao uwezo wao wa kujimudu kimaisha umepungua au haupo kabisa na hakuna mtu wa kuchukua jukumu hilo. Kutokana na hali hiyo jamii husika inawajibika kutoa matunzo kwa watu hao. Matunzo ya watu wenye ulemavu katika makazi (Institution based care) yatakuwa kimbilio la mwisho baada ya njia zingine kushindikana.

**Tamko la Sera:**

| | |
|---|---|
| (i) ) | Serikali kupitia Halmashauri za Wilaya na Wakala za Hiari itaendelea kutoa na kuboresha matunzo kwa watu wenye ulemavu/wasiojiweza katika makazi. |
| (ii) | Serikali kushirikiana na wakala za Hiari itaweka utaratibu wa kuhamasisha ndugu, familia na jamii juu ya wajibu wao wa kuwatunza ndugu zao wenye ulemavu. |

### 3.13 Hoja ya Sera: Huduma kwa Watu wenye Ulemavu katika Jamii (Community Based Rehabilitation - CBR).

Utaratibu wa utoaji wa huduma za marekebisho kwa watu wenye ulemavu katika taasisi una kasoro zifuatazo:

(i) Unahudumia watu wachache.
(ii) Unawatoa wahudumiwa nje ya eneo lao la asili.
(iii) Unawatenga wahudumiwa na jamii.
(iv) Unaleta uwezekano wa unyanyapaa.

Kwa upande mwingine utoaji wa huduma za marekebisho kwa watu wenye ulemavu katika jamii (CBR) unaleta faida zifuatazo:

(i) Unahudumia watu wenye ulemavu wengi na wa aina mbalimbali kwa wakati mmoja.
(i) Haumtoi mlengwa katika eneo lake la asili.

(iii) Unajumuisha wasio na ulemavu katika utekelezaji.

(iv) Unajenga mshikamano baina ya watu wenye ulemavu na wananchi wengine hivyo kuondoa dhana ya unyanyapaa.

**Tamko la Sera.**

| |
|---|
| Utaandaliwa utaratibu utakaohakikisha kwamba utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu katika jamii (CBR) unakuwa ni mkakati na njia kuu ya upatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu katika jamii. |

**3.14 Hoja ya Sera: Mchangamano katika Jamii.**

Mchangamano ni kiwango cha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maisha na kazi za jamii. Dhana ya mchangamano imejumuisha taratibu za utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu kwa kutumia taasisi na vyombo vile vile vinavyotumiwa na watu wasio na ulemavu.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utaandaliwa utaratibu utakaohakikisha kwamba Asasi na vyombo mbalimbali vinavyotoa huduma kwa wananchi vinatoa huduma zao kwa watu wenye ulemavu kama wanavyozitoa kwa watu wasio na ulemavu isipokuwa pale panapolazimu huduma maalum. |

**3.15 Hoja ya Sera: Michezo.**

Michezo ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu. Kushiriki katika michezo kunamwezesha mshiriki:

(i) Kujenga na kukomaza afya ya mwili na akili.

(ii) Kujenga ukakamavu, nidhamu na uwezo wa kujihami.

(iii) Kuonyesha uwezo na vipaji.

(iv) Kukuza na kuendeleza uhusiano wa kirafiki baina ya jamii mbalimbali.

Kwa mantiki hii watu wenye ulemavu kama watu wengine wasio na ulemavu wana haki ya kushiriki katika michezo. Isitoshe michezo ni tiba kwa watu wenye ulemavu kwa sababu kasoro za kimwili na kiakili zinarekebishwa kwa kushiriki katika michezo na burudani.

**Tamko la Sera:**

Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanashiriki kwa ukamilifu katika shughuli za michezo na burudani. Aidha utaandaliwa utaratibu utakaoshirikisha vyama vya michezo na wadau wengine kuhakikisha kwamba shughuli za michezo kwa watu wenye ulemavu zinakuwa sehemu ya mpango wa kuendeleza michezo kitaifa.

## 3.16 Hoja ya Sera: Dini.

Dini ni haki ya msingi kwa binadamu bila kujali jinsi na hali yake.

Ushiriki katika dini unamwezesha binadamu kupata amani na kuwa na mahusiano mema na binadamu wengine.

**Tamko la Sera:**

(i) Taasisi na mashirika ya dini yatahakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanashiriki kwa ukamilifu katika shughuli za dini.

(ii) Taasisi na mashirika ya dini yatahamasishwa ili kuhakikisha kwamba majengo ya Ibada yanaingilika bila vikwazo na taarifa zinazohusiana na dini zinawafikia watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

## 3.17 Hoja ya Sera: Usafiri na Usalama Barabarani.

Watu wenye Ulemavu wanakabiliwa na matatizo mbalimbali katika nyanja ya usafiri. Muundo wa vyombo vya usafiri hauruhusu kuingia na kutoka kwa urahisi watu wenye ulemavu. Kadhalika barabara zimejengwa pasipo kuzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu.

**Tamko la Sera:**

(i) Utaandaliwa utaratibu utakaowashirkisha wadau kuhakikisha kwamba vyombo vya usafir vinaruhusu utumiaji wa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaweka utaratibu utakaohakikisha kwamba barabara zinakuwa na vifaa na alama zitakazosaidia usalama wa watu wenye ulemavu katika kutumia barabara hizo.

## 3.18 Hoja ya Sera: Ajali na Fidia.

Watu wanaopata ulemavu kutokana na ajali kwenye vyombo vya usafiri na sehemu za kazi wanakabiliwa na tatizo la kutopata fidia na pale fidia inapotolewa huwa ni ndogo isiyolingana na ulemavu waliopata na matarajio mema ya baadaye.

Pamoja na kuwepo sheria ya fidia kwa ajali inayompata mtu akiwa kazini (workmans compensation), sheria hiyo ina mapungufu kwa kuwa haiwahusishi watu walio katika sekta isiyo rasmi wasioajiriwa. Aidha fidia hutolewa kwa baadhi ya viungo vya hivyo mwajiriwa akiumia kiungo ambacho hakikutajwa bado hana stahili ya kupata fidia.

**Tamko la Sera:**

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengne itafanya mapitio ya sheria ya fidia kwa lengo la:-

(i) Kuhakikisha kwamba fidia inayotolewa inakidhi mahitaji ya mfidiwa aliyepata ulemavu.

(ii) Kubadilisha kigezo chafidia kuwa athari aliyopata mfidiwa bila kujali kiungo alichoumia.

### 3.19 Hoja ya Sera: Haki na Ulinzi wa Kisheria.

Watu wenye ulemavu kama wananchi wengine wanayo haki ya kuheshimiwa, kutobaguliwa, kupata ajira na matunzo. Pamoja na haki hizo jamii imekuwa na mazoea ya kuwanyima watu wenye ulemavu haki zao kutokana na unyanyapaa.

**Tamko la Sera:**

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itafanya mapitio na marekebisho ya sheria zisizolinda na kutoa haki kwa watu wenye ulemavu.

### 3.20 Hoja ya Sera: Mafunzo ya Watumishi.

Huduma kwa watu wenye ulemavu zinahitaji watumishi wenye elimu na ujuzi wa kutosha. Watumishi walio wengi hawana taaluma husika na hawapati mafunzo ya mara kwa mara.

**Tamko la Sera:**

(i) Serikali, Taasisi na wakala za Hiari zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu zitaandaa taratibu zitakazowawezesha watumishi kupata taaluma na ujuzi unaohitajika.

(ii) Utaandaliwa utaratibu kuhakikisha kwamba watumishi/ wanaohudumia watu wenye ulemavu wanapata taaluma na ujuzi unaohitajika.

**3.21 Hoja ya Sera: Habari, Takwimu na Tafiti.**

Habari sahihi na takwimu ni nyenzo muhimu katika upangaji na utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Pamoja na umuhimu huo eneo la huduma kwa watu wenye ulemavu linakosa taarifa na takwimu muhimu zinazoweza kutumika katika mipango ya utekelezaji wa huduma hiyo.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Ili kundoa kasoro hii utawekwa utaratbibu utakaohamasisha taasisi za Serikali, watu binafsi na wakala za Hiari (Ngo's) za ndani na nje ya nchi zishiriki kikamilifu katika kufanya tafiti katika eneo hili la huduma. |

**3.22 Hoja ya Sera: Vyama vya Watu Wenye Ulemavu.**

Upo umuhimu wa kuwepo vyama vya watu wenye ulemavu ili kuwakilisha na kujisemea katika ngazi mbalimbali, kufanya utambuzi wa mahitaji yao pia kutathmini huduma zinazotolewa na kuchochea maendeleo yao.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| **Utawekwa utaratibu wa kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya watu wenye ulemavu na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.** |

**3.23 Hoja ya Sera: Vyama vya Hiari vya Kuhudumia Watu wenye Ulemavu.**

Serikali inatambua umuhimu wa huduma zinazotolewa na taasisi na vyama vya hiari vinavyohudumia watu wenye ulemavu. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hizo na itahakikisha kwamba huduma zinazotolewa zinazingatia viwango vinavyotakiwa.

Utaratibu wa sasa wa kusajili vyama vya hiari vinavyotoa huduma kwa watu wenye ulemavu una mapungufu makubwa kwa sababu Wizara inayohusika na huduma hizo haina uwezo wa kukagua utendaji kazi wa wakala hizo. Ili kurekebisha kasoro hizi:-

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu unaohakikisha kwamba:-<br>(i) Usajili wa vyama vya kuhudumia watu wenye ulemavu unapitia Wizara inayohusika na watu wenye ulemavu.<br>(ii) Usajili wa vyama hivyo hauambatani na ruhusa ya kutoa huduma na kwamba Wizara inayohusika na huduma hiyo itoe ruksa (license) ya kutoa huduma.<br>(iii) Serikali itaratibu shughuli za wakala za hiari zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu kwa lengo la kuboresha huduma hizo. |

**3.24 Hoja ya Sera: Mfuko wa Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu.**

Watu wenye ulemavuni miongoni mwa watu maskini katika jamii. Kadhalika ni nguvu kazi kubwa ambayo haijatumika. Watu wenye ulemavu hawajapewa fursa ya kupata na kutumia Rasilimali zinazoweza kuwaletea maendeleo ili kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Upo umuhimu wa kuweka mazingira yatakayowawezesha watu wenye ulemavu kushiriki, kupata na kutumia vyombo vinavyohusika na uzalishaji mali vilivyopo ili kujiletea maendeleo.

**Tamko la Sera:**

| |
|---|
| Serikali itaanzisha mfuko utakaowawezesha watu wenye ulemavu kujijengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali kwa ajili ya maendeleo yao. |

**3.25 Hoja ya Sera: Ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu na vinavyohudumia watu wenye ulemavu.**

Vyama vya watu wenye ulemavu na vinavyohudumia watu wenye ulemavu vinanafasi kubwa katika kuimarisha mshikamano na kuchochea maendeleo miongoni mwa watu wenye ulemavu. Pamoja na umuhimu huo Asasi hizi hazina fedha za kuweza kujiendesha bali kutegemea misaada toka kwa wahisani. Kutokana na kazi kubwa wanazozifanya, Serikali inawajibu wa kuzitambua na kuzipa moyo ili ziweze kuendelea na kazi hii.

**Tamko la Sera.**

| |
|---|
| Utawekwa utaratibu utakaohakikisha kwamba vyama vya watu wenye ulemavu vya kuhudumia Watu wenye ulemavu vinapewa ruzuku kama motisha kwa huduma wanazozitoa. |

**3.26 Hoja ya Sera: Ushirikiano wa Kimataifa.**

Eneo la huduma kwa watu wenye ulemavu ni jipya katika maendeleo ya nchi yetu. Uwezo tulionao ki rasilimali/kiuzoefu hautoshelezi kukidhi mahitaji ya kuleta maendeleo na utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu. Upo umuhimu kwa Tanzania kujifunza kutoka katika nchi zenye uzoefu katika eneo hili la huduma. Aidha Tanzania kama sehemu ya jumuiya ya kimataifa tunalalzimika kushirikiana na mataifa mengine.

**Tamko la Sera.**

| |
|---|
| Serikali itaendeleza uhusiano wa kimataifa na taasisi mbalimbali, mashirika yaliyo Chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa ilikuendeleza na kuboresha huduma kwa Watu wenye ulemavu nchini. |

## SURA YA NNE.

### 4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU.

Watu wenye ulemavu wanayo haki na nafasi ya kujiendeleza na kupata huduma katika jamii sawa na watu wasio na ulemavu. Ushiriki wa watu wenye ulemavu katika maisha ya kila siku katika jamii hauna budi kulenga katika kupunguza au kuondoa maisha ya utegemezi.

Ili kuleta maendeleo na kuboresha huduma kwa watu wenye ulemavu, mgawanyo wa majukumu katika utekelezaji wa sera hii utakuwa kama ifuatavyo:-

### 4.1 Serikali Kuu.

- Kusimamia utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu.
- Kuboresha sheria zinazohusu maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu.
- Kuhakikisha kuwepo kwa ushiriki, mchangamano na usawa wa fursa kwa watu wenye ulemavu katika maisha yao na ya jamii.
- Kuhimiza Halmashauri za wilaya, Serikali za mitaa na Wakala za Hiari ili zitoe huduma kwa watu wenye ulemavu.

### 4.2 Serikali za Mitaa.

- Kufanya utambuzi na kujua mahitaji ya watu wenye ulemavu katika jamii.
- Kutoa matunzo na ulinzi kwa watu wenye ulemavu.
- Kuwapa mahitaji muhimu ya maisha kulingana na hali zao.
- Kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika mipango ya uzalishaji mali na utekelezaji wake.
- Kufanya utambuzi wa wakala za Hiari zinazotoa huduma kwa watu wenye ulemavu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za wakala hizo.

### 4.3 Familia/Vijiji.

- Kwa kushirikiana na Serikali za mitaa na wakala za Hiari familia/vijiji vitatoa matunzo na ulinzi kwa watu wenye ulemavu.
- Kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa/Wakala za Hiari, familia/vijiji vitashiriki katika kupanga na kutekeleza shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kuinua kipato.

### 4.4 Wakala za Hiari.

- Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya Wakala za Hiari zitafanya utambuzi kwa lengo la kujua mahitaji ya Watu wenye ulemavu.
- Kushirikiana na Serikali za mitaa katika kutoa misaada ya maisha kwa watu wenye ulemavu.
- Kutoa matunzo na ulinzi kwa watu wenye ulemavu.
- Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Wakala za Hiari zitahamasisha na kuhakikisha ushiriki wa watu wenye ulemavu na familia zao katika mipango ya uzalishaji mali na utekelezaji wa shughuli za uzalishaji mali.